# FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI: MBINU YA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZA KUSOMA NA KUANDIKA

***Stella Faustine***
*Chuo Kikuu cha Dodoma - Tanzania*
*stelafau@gmail.com*

***Said Waziri***
*Shule ya Sekondari Njoro, Kiteto - Tanzania*
*wazirsai@gmail.com*

## Ikisiri

*Katika historia ya fasihi ya Kiswahili, fasihi ya watoto, haina muda mrefu ikilinganishwa na fasihi ya watu wazima. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili ilitelekezwa kwa muda mrefu kutokana na wahakiki kutoipa umuhimu unaostahili na hivyo kudharauliwa na wanajamii. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 2000 mpaka hivi sasa, kumekuwa na msukumo mkubwa kwa watafiti mbalimbali kufanya tafiti zao kwa kuimakinikia fasihi hiyo. Miongoni mwa mambo yaliyoshughulikiwa ni nafasi ya fasihi katika kumkuza mtoto kisaikolojia, sifa bainifu za fasihi ya watoto, uhusiano wa fasihi ya watoto na umilisi wa kusoma pamoja na mbinu zinazotumika kufundisha fasihi ya watoto. Katika mijadala hiyo, fasihi ya watoto, mahususi kipera cha nyimbo hakijamakinikiwa kama mbinu msingi ya kujifunzia kusoma na kuandika. Jambo hili limeacha pengo la kimaarifa ambalo limezibwa na utafiti uliozalisha makala hii kwa kubainisha ni kwa namna gani fasihi ya watoto (kwa kutumia kipera cha nyimbo), inaweza kutumika kama mbinu msingi ya kufundishia stadi za kusoma na kuandika. Aidha, utafiti uliozalisha makala hii ni wa kitaamuli. Data zilipatikana maktabani kwa kutumia mbinu ya mapitio ya nyaraka. Data zilikusanywa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia Nadharia ya Utabia. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa fasihi ya watoto, mahususi kipera cha nyimbo ina umuhimu mkubwa katika kufunza stadi za kusoma na kuandika.*

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya watoto ni aina ya fasihi iliyoandikwa kwa kuwalenga watoto[22] kama hadhira lengwa. Fasihi hiyo inaweza kuwa imetungwa na watoto au watu wazima lakini ikiwakusudia watoto kuwa watendaji wakuu. Fasihi ya watoto inaweza kuwa nyimbo, hadithi, visakale au vibonzo ambavyo hujengwa katika lugha rahisi, visa vichache na mambo mema ambayo hutazamwa kama matarajio makuu. Vitendo huwa na msuko sahili, pamoja na matumizi ya fantasia kwa kiwango kikubwa (Jolongo, 2014).

Historia ya fasihi ya watoto inakadiriwa kuwapo ulimwenguni zaidi ya miaka 1000 iliyopita, ambapo inasadikiwa kuwa masimulizi ya kingano ndiyo yaliyojenga msingi wa fasihi ya watoto ya zamani. Masimulizi hayo yalikusudiwa kutimiza jukumu la kuburudisha, kuiunganisha jamii pamoja na kuwafunza vijana namna ya kuishi kwa kufuata misingi ya dini zao za jadi na kuwarithisha mila na tamaduni za jamii zao. Darton (1982) anafafanua kuwa katika jamii za Kimagharibi, fasihi ya watoto ilitokana na utamaduni wa Wagiriki na Warumi, hasa katika kipindi cha miaka ya 500KM na 400BM. Katika kipindi hiki, watoto walikuwa na simulizi zao ambazo hazikuwa na maudhui mazito zaidi ya kuwaburudisha. Wasimulizi wengi walisimulia hadithi za watoto zilizokusudia kufunza maadili kama silaha ya kujenga amani, mshikamano na pia kuleta maendeleo kwa jamii. Baadaye, katika miaka ya 1400, mataifa ya Ulaya yaliingia katika kipindi cha mvuvumko mpya (*new renaissance*), ambapo kazi za fasihi, falsafa na dini zilizaliwa upya. Katika kipindi hiki, kama anavyoendelea kufafanua Darton (Keshatajwa), vitabu vya fasihi ya watoto vilianza kuandikwa huku maudhui yake yakilenga kurekebisha tabia za watoto baada ya machafuko na umwagaji damu kutokea huko Ulaya, yaliyosababishwa na machafuko ya kidini.

Barani Afrika, fasihi ya watoto ilikuwapo tangu zamani lakini haikuwa katika umahususi wake. Iliwajumuisha watu wa rika zote, kuanzia wakubwa

[22] Mtu/Watu wenye umri chini ya miaka 18 (BAKITA, 2017).

na hata watoto. Kama simulizi, ilikuwa ni hadithi au bunilizi ya aina yoyote; basi ilifaa kwa hadhira yote, yaani watoto na watu wazima. Fasihi hii ilikuwa ya masimulizi ambayo iliwasilishwa kwa njia ya hadithi, visasili, nyimbo, tendawili na nahau (Ngugi, 2009)Kwa upande wa fasihi ya watoto iliyoandikwa, tunaweza kusema kuwa, ni changa kwa maana kuwa imeibuka hivi karibuni. Hii inatokana na ukweli kwamba, barani Afrika, fasihi ya watoto inayowahusu watoto wenyewe kwa umahususi, haikuanza muda mrefu kama fasihi nyingine.

Tafiti zinaonesha kwamba, fasihi ya watoto iliyo katika umahususi imechipuka kuanzia miaka ya 1980 kutokana na sababu kadhaa. Miongoni mwazo ni kutiliwa mkazo kwa masuala ya haki za watoto (Ngugi, 2010). Katika kipindi hicho, fasihi ya watoto iliyojulikana zaidi katika bara la Afrika ni ile iliyokuwa katika masimulizi na nyimbo (Omari, 2009). Tanzu zingine za fasihi ya watoto zilikuwapo lakini hazikupewa nafasi kubwa. Mulokozi (2017) anasema kuwa kabla ya miaka ya 1990, fasihi ya watoto ya Kiswahili ilikuwa ile isiyokuwa rasmi, iliyokuwa katika mtindo wa ngano na hadithi. Hadithi hizo ingawa zilikuwa zinanasibishwa na watoto, pia ziliwafaa watu wazima. Hii ni sawa na kusema kuwa, kulikuwa na mstari mwembamba sana wa kuitofautisha fasihi ya watoto ya Kiswahili na ile ya watu wazima.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, fasihi ya watoto iliyowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili ilionekana kupiga hatua zaidi nchini Kenya ambapo ilijumuishwa katika muhtasari wa somo la Kiswahili (Bakize na wenzake, 2017). Nchini Tanzania, Mulokozi (2017) anafafanua kuwa licha ya fasihi ya watoto kukua katika mawanda ya kidunia, bado haikupewa nafasi ya kutosha. Hata hivyo, kukua kwa fasihi ya watoto katika mawanda ya kidunia, kumetoa msukumo kwa watafiti mbalimbali kufanya tafiti zao kwa kuimakinikia fasihi ya watoto. Miongoni mwa watafiti hao ni Jalongo (2014) ambaye ameeleza umuhimu wa vielelezo katika mchakato mzima wa kusoma kwa watoto. Anabainisha kuwa, vielelezo vinavyopatikana ndani ya kazi za fasihi za watoto hubainisha ujuzi mwingine ambao watoto huupata kutokana na msaada wa vielelezo hivyo. Anataja ujuzi huo kuwa ni wa

kutazama ambao hutokana na kuangalia vielelezo, kutambua maana yake, utafutaji wa taarifa zilizotajwa katika andiko na ujuzi wa lugha pale ambapo hupewa majina, matumizi ya misamiati mipya, mishangao inaposemwa kwa sauti na watoto kuanza kujifunza kusoma na kuandika. Umuhimu wa vielelezo kama mbinu msingi ya kuwasilisha maudhui kwa watoto unafafanuliwa pia na Shima (2012). Katika andiko lake, anaweka bayana kuwa katika fasihi ya watoto, vielelezo vina nafasi kubwa katika kueleweka kwa maudhui yaliyomo ndani yake. Hii ni kwa sababu hutoa msaada wa kiufafanuzi wa yale yaliyomo ndani ya matini, husaidia kumjenga kimaadili, na pia husaidia kupanua fikra za mtoto.

Wataalamu wa fasihi wamebaini kuwa katika Afrika Mashariki fasihi ya watoto inayojulikana zaidi ni ile ya nyimbo zinazoimbwa na watoto (Bakize, 2014). Tanzu nyingine kama vile ushairi, riwaya na tamthiliya bado hazijafahamika vyema. Kutofahamika kwa tanzu hizo ni sababu mojawapo inayosababisha fasihi ya watoto isipewe umuhimu katika jamii. Bakize Keshatajwa) anaendelea kufafanua kuwa hali hii haiidunishi fasihi ya watoto peke yake, bali pia, inatoa nafasi kwa watafiti kufanya tafiti mbalimbali kuhusiana na fasihi hiyo.

Mchango wa fasihi ya watoto kama mbinu ya kukuza maarifa mapya umebainishwa na wataalamu mbalimbali kwa viwango tofauti. Chacha (2016) anafafanua kuwa fasihi ya watoto ina nafasi kubwa ya kumfunza mtoto lugha. Mtazamo wa mtafiti huyu umekitwa katika mawanda ya fasihi ya watoto kwa jumla na siyo katika umahususi wa kuangalia kipera kimojawapo kati ya vipera vingi vya fasihi ya watoto. Katika upana huu wa kimawanda, Abdallah (2018) anaitazama fasihi ya watoto ya kidijiti kama nyenzo muhimu katika kukuza fasihi simulizi huku akitoa mifano kutoka vibonzo jongevu. Kwa jumla, anabainisha kipera cha nyimbo kama njia ya kufundishia alfabeti za Kiswahili (A- Z). Anasisitiza kuwa nyimbo ni njia nzuri ya kuwakaririsha wanafunzi kile wasichokijua; yaani, maarifa mapya. Maelezo haya yalikuwa ya msingi sana katika utafiti huu kwa sababu mbili. Mosi, yanathibitisha kuwapo kwa matumizi ya nyimbo kama mbinu ya

kufundishia maarifa mapya. Pili, yanathibitisha urahisi unaopatikana kwa kutumia nyimbo kuwafundishia watoto maarifa mapya. Hata hivyo, maelezo haya yameegemezwa zaidi katika kutazama nyimbo kama mbinu inayosisitiza jambo fulani katika kazi za vibonzo jongevu tu. Hayaoneshi kuwa nyimbo hizo zinaweza kutumika pia kama mbinu msingi ya kufundishia kusoma na kuandika darasani. Kauli hii ya Abdallah (Keshatajwa), kuwa nyimbo hutumiwa kufundishia alfabeti za Kiswahili, ni ushahidi tosha kuwa kufundisha alfabeti kwa kutumia nyimbo kutamsaidia sana mtoto kusoma na kuandika. Hivyo, utafiti huu ulilazimika kuichunguza nafasi ya fasihi ya watoto ya Kiswahili ili kuziba pengo lililobainishwa hapo juu.

Kwa mujibu wa TET (2016 na 2018) nyimbo zinafaa kutumika katika kutekeleza jukumu la ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika kwa madarasa ya awali. Hata hivyo, TET (Keshatajwa) haijafafanua ni kwa namna gani nyimbo hizo zinaweza kurahisisha au kufanikisha suala zima la ujifunzaji wa stadi hizo kwa watoto. Pia, haijaweka bayana ni nyimbo zipi zinazofaa kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi kama mwongozo kwa walimu.

Kwa ujumla, kama inavyoonekana katika mapitio ya maandiko yaliyofanywa na wataalamu tajwa hapo awali, tafiti nyingi zimebainisha umuhimu wa fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa ujumla na si kwa kuitazama moja kwa moja kama mbinu msingi ya kufundishia na kujifunzia stadi za lugha. Mwanya huu wa kimaarifa ulioachwa na watafiti hao, ndio unaotoa msukumo kwa waandishi wa makala hii kubainisha ni kwa namna gani fasihi ya watoto ya Kiswahili inavyoweza kuziba ombwe la tatizo la kujua kusoma na kuandika, mahususi kwa kutumia kipera cha nyimbo. Hivyo, makala hii inatoa mwanga kwa walimu, wazazi na wadau mbalimbali katika sekta ya elimu, kuutazama utanzu wa fasihi kama mbinu mwafaka inayoweza kufunza maarifa katika ngazi mbalimbali kwa jamii.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Mjadala wa makala hii umeongozwa na Nadharia ya Utabia ambayo imeasisiwa na Watson na wenzake (2012). Msingi mkuu wa nadharia hii ni ule unaofafanua kuwa mtu anaweza kujifunza jambo lolote lile pasipo kujali uwezo wake wa asili. Anasisitiza kuwa ujifunzaji wa stadi mbalimbali ikiwamo kusoma na kuandika ni mwigo unaotokana na mazingira halisi ya mwanadamu. Hoja hii imeendelezwa na Skinner (1957) kwa kufafanua kuwa licha ya ujifunzaji wa stadi mbalimbali, mwigo pia ni uimarishaji wa tabia unaojengwa na vitia motisha mbalimbali. Anasisitiza kuwa katika tendo la ufunzaji na ujifunzaji vitia motisha chanya huchochea mwendelezo wa tendo la ujifunzaji kwa kujirudia tena na tena. Vitia motisha hasi hupunguza urejelewaji wa tendo la kujifunza. Kwa mujibu wa Khakasa (2018), nadharia hii imejengwa na mihimili saba. Nayo kama ilivyotumika katika mjadala wa makala hii ni:

i. Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ufanywe kwa kukariri na kurudiarudia matamshi ya vipande vya mazungumzo (tamthiliya ndogo) na miundo ya sentensi. Mhimili huu umesaidia kubaini umuhimu wa kurudiwa na kukaririwa kwa maneno au matamshi katika nyimbo kama mbinu msingi ya kujifunza kusoma na kuandika.

ii. Tabia nzuri katika kujifunza lugha ya pili hujengeka vizuri ikiwa mwanafunzi ataelekezwa vizuri kutofanya makosa. Mhimili huu ulitumiwa kubainisha motisha hasi ambazo hutolewa kupitia nyimbo ili kumkanya mtoto ambaye hapendi kujifunza, na kumfanya awe na mwelekeo chanya katika kujifunza kusoma na kuandika.

iii. Stadi za lugha zifanywe kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza kwanza kabla ya kusoma na kuandika. Mhimili huu umesaidia kubaini namna usikilizaji na utamkaji wa maneno kupitia nyimbo unavyorahisisha tendo la kujifunza kusoma na kumwezesha mwanafunzi kukariri na kutamka maneno kabla ya kuandika.

iv. Ufundishaji wa sarufi na vipengele vingine vya lugha usifanywe kwa kuchambua vipengele vya lugha. Mwanzoni wanafunzi wakariri kwa kurudia na kuiga vipengele hivyo na kuvizoea kutoka katika vitabu vya hadithi. Wakifanya hivyo, watang'amua wao wenyewe kwa njia ya kukisia kanuni zinazotawala lugha.

v. Ujifunzaji wowote ule ni matokeo ya uimarishaji wa tabia unaosababishwa na vitia motisha ambavyo husaidia tabia fulani kujirudiarudia ama la. Mhimili huu ulisaidia kubaini namna nyimbo kama kitia motisha, unavyosaidia kuchochea tendo la ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za lugha za kusoma na kuandika.

vi. Mwanafunzi anapaswa kufuata maagizo ya mwalimu na jukumu la mwalimu ni kusimamia utekelezaji wa maagizo anayoyatoa darasani. Mhimili huu ulisaidia kubaini namna maelekezo ya mwalimu katika kuongoza nyimbo mbalimbali darasani, yanavyoweza kuimarisha tendo la kujifunza kusoma na kuandika.

vii. Kujifunza lugha ni sawa na kujenga ujuzi wa vipashio vya lugha, kama vile fonimu, mofimu, na vifungu vya maneno. Msingi huu ulisaidia kupata uelewa ni namna gani wimbo unavyoweza kufundisha vipashio mbalimbali vya lugha ambavyo huwezesha kuunda silabi, neno, sentensi na hatimaye vifungu vya maneno.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Mjadala katika makala hii umefanywa kwa kuzingatia misingi ya kitaamuli. Data zilikusanywa maktabani na uwandani kisha kuchanganuliwa na kuwasilishwa kama matokeo ya utafiti kwa kutumia mbinu ya maelezo. Aidha, uwasilishwaji wa matokeo ya utafiti ulihusisha tafakuri binafsi, taarifa mbalimbali za kitafiti, nadharia husika pamoja na data zilizopatikana maktabani kama inavyofafanuliwa na Ponera (2019). Sampuli iliyotumika katika upatikanaji wa data ni sampuli lengwa ya kipekee ambayo ilizingatia sifa zinazofaa za watafitiwa na vitafitiwa vinavyohusiana na mada husika. Aidha, sehemu ya data za utafiti huu zimetokana na utafiti uliofanywa katika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya mahitaji ya kukamilisha

shahada ya umahiri katika fasihi ya Kiswahili (2020) wenye mada isemayo: "Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Kukuza Stadi za Kusoma na Kuandika." Aidha, nyimbo za watoto zimepewa majina kulingana na maudhui yanayopatikana ndani ya wimbo husika.

## 4.0 Namna Nyimbo Zinavyotumika Kufundishia Kusoma na Kuandika

Katika fasihi ya Kiswahili ya watoto, zipo nyimbo mbalimbali ambazo huimbwa na watoto katika mazingira yasiyo rasmi, yaani majumbani na yale yaliyo rasmi, yaani shuleni. Kwa upande wa mazingira ya nyumbani, nyimbo hizi huimbwa kwa ujumla kama sehemu ya burudani. Shuleni, nyimbo hizi hutumika kufundisha na kujifunza kusoma na kuandika. Nyimbo zinazotumika kufundishia kusoma na kuandika zimegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni nyimbo zinazoamsha ari ya kujifunza kusoma na kuandika na kundi la pili ni nyimbo zinazofunza stadi za kusoma na kuandika. Makundi haya yamefafanuliwa kama ifuatavyo:

### 4.1 Nyimbo Zinazoamsha Ari ya Kujifunza Kusoma na Kuandika

Nyimbo zinazoamsha ari ya kusoma na kuandika hazihusiki moja kwa moja na tendo la kufundisha au kujifunza kusoma na kuandika. Walimu hutumia nyimbo hizi shuleni kwa sababu kuu mbili. Sababu ya kwanza ni kuwajengea wanafunzi ari na moyo wa kupenda shule. Wanafunzi wanaoanza kujifunza kusoma na kuandika, wengi wao huwa bado wana umri mdogo. Kitendo cha kubadili mazingira kutoka nyumbani na kwenda katika mazingira ya shule kinaweza kusababisha hali mbili kinzani kutokana na namna watakavyoyapokea mazingira hayo. Wapo watakaopenda mazingira ya shule na hivyo kuwa tayari kusoma pasipokuwa na usumbufu; lakini pia, wapo wale ambao mazingira mapya yanaweza kuwa siyo rafiki kwao. Kama Nadharia ya Utabia inavyotuelekeza kuwa utoaji motisha ni mbinu mojawapo inayochochea tabia fulani kuimarika na kumfanya mtu kupenda jambo fulani. Katika mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, jukumu la mwalimu ni kutengeneza mazingira rafiki yatakayomvuta mwanafunzi kujisikia kuwa yuko katika mazingira salama na hivyo kumwezesha kukaa kwa utulivu. Kwa mfano, kwa wanafunzi wa elimu ya awali, nyimbo mbalimbali hutumika kama motisha ili kuamsha moyo wa kupenda mazingira na kuwajengea utulivu. Miongoni mwa nyimbo zinazoimbwa ni huu ufuatao:

**Maua Mazuri**

*Maua mazuri yapendezaaa*
*Ukiyatazama yanameremetaa*
*Waite watoto waende shule*
*Zum, zum, zum nyuki lia weee ×2*
*Toka mbali kutafuta ua zuri kwa chakula*
*Hesabu ni nzuri sana weee*
*Mwalimu nifundishe, siwezi kusahau*
*Ee mwalimu, ee mwalimu nifundisheee*
*Jogoo lawika kuamsha wajinga*
*Waliolala waende shuleni*
*Zum, zum, zum nyuki lia weee ×2*
**Chanzo**: Waziri (2020)

Uimbaji wa wimbo huu huenda pamoja na vitendo. Wanafunzi hurukaruka, hupiga makofi, huchezesha viungo vya mwili na huchangamana na wengine. Hali hii huwafanya kufurahi, kuwajengea ujasiri na imani katika mazingira mapya wanayokuwamo. Ujasiri anaoupata mototo kutokana na nyimbo anazoimba humfanya kuzoea mazingira haraka, kupenda shule na hivyo hujifunza kusoma na kuandika kwa kujiamini.

Licha ya nyimbo kujenga ari ya kupenda mazingira ya shuleni, hutumka pia kama kitia motisha kinachoweza kuamsha ari ya kupenda kusoma na kuandika kwa mwanafunzi. Hii ni kwa sababu zipo nyimbo zenye maudhui yanayomfanya mwanafunzi apate ujumbe kuhusu uzuri au ubaya wa kutojua kusoma na kuandika. Mfano mzuri wa wimbo unaoamsha ari ya kutaka kujua kusoma na kuandika ni kama ufuatao:

**Asiyependa Shule**

*Asiyependa shule ni mjinga kabisa* x 2
*Barua ikija atembeza pote* x 2
*Huyo huyo ni mjinga kabisa* x 2
**Chanzo**: Waziri (2020)

Wimbo huu una dhima kubwa katika suala zima la ujifunzaji wa kusoma na kuandika. Kwanza, ni kitia motisha kinachomfanya mwanafunzi kuwa na ari ya kupenda shule kutokana na burudani anayoipata. Pili, kwa kuzingatia Nadharia ya Utabia kuwa tabia nzuri katika kujifunza hujengeka vizuri ikiwa mwanafunzi ataelekezwa vizuri kutofanya makosa, wimbo huu unamfunza kutokufanya makosa ya kutopenda shule kwa kufafanua madhara yake. Hii ni kutokana na athari za ujinga ambazo zinawasilishwa kama madhara yatakayompata mtu asiyependa shule: "*Asiyependa shule ni mjinga kabisa*". Kwa hiyo, kutokana na wimbo huu mwanafunzi atajenga dhana akilini mwake kuwa kutokujua kusoma ni ujinga; hivyo asipojua kusoma atakuwa mjinga. Ili kuepuka kuwa mjinga ni sharti aende shule ambako kwa kufanya hivyo ataweza kujifunza stadi za kusoma na kuandika. Tatu, wimbo huu unaamsha ari ya mwanafunzi ya kutaka kujifunza kusoma na kuandika. Kipengele kinachosema, "*Barua ikija atembeza pote*" kinaibua hisia za udhalilikaji ndani yake. Hivyo, ili kupambana na hali hiyo kutaibuka ari ya kutaka kujua kusoma na kuandika. Nyimbo hizi huimbwa kabla ya kuanza mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na baada ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu ndiye atakayeamua ni wakati gani aanzishe wimbo ili kufanikisha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji darasani. Lengo la nyimbo hizi ni kuwaandaa wanafunzi kuwa na utayari wa kujifunza. Pia, nyimbo hizi huongeza morali ya kuyapenda mazingira ya kujifunzia.

### 4.2 Nyimbo za Kufundishia Stadi za Kusoma na Kuandika

Kumudu stadi za kusoma na kuandika ni kitendo ambacho huhusisha mchakato mrefu. Zipo hatua mbalimbali ambazo mwanafunzi hupitia mpaka kuweza kusoma na kuandika herufi mbalimbali. Walimu wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali ili kukamilisha tendo hilo. Miongoni mwazo kama zinavyoelezwa na TET (2016) ni: onesho mbinu, hadithi, nyimbo, ngonjera, michezo, na maswali na majibu. Sehemu hii inabainisha kwa umahususi namna nyimbo zinavyoweza kutumika kufundishia kusoma na kuandika. Aidha, utafiti uliozalisha makala hii umebaini kuwa miongoni

mwa nyimbo zinazotumika kufundishia kusoma na kuandika ni zile zinazowaelekeza wanafunzi kuumba herufi kwa kuzifananisha na maumbo ya vitu halisi, wanyama au viungo mbalimbali vya mwili wa binadamu. Nazo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Nyimbo za Kufundishia Stadi za Kusoma

TET (2016) inafafanua kuwa kusoma ni kitendo cha kutazama na kutambua herufi na maneno yaliyoandikwa. Tendo la kusoma hufanywa kwa namna mbili. Mosi ni kusoma kwa sauti, na pili ni kusoma kimyakimya. Kwa kutumia nyimbo, wanafunzi hujifunza kusoma kwa sauti kupitia mbinu mbalimbali za ujifunzaji. Mbinu ya kwanza ni kusikiliza maneno na kuyatamka kupitia nyimbo mbalimbali. Khakasa (2018) anafafanua kuwa stadi za lugha zinapaswa kufundishwa kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza kabla ya kusoma na kuandika. Katika mantiki hii, na kama ambavyo tunaelekezwa katika Nadharia ya Utabia kuwa katika kujifunza stadi za lugha haina budi kuanza kusikiliza na kuzungumza kabla ya kusoma na kuandika. Hivyo, ni dhahiri kuwa nyimbo ni mbinu mwafaka katika ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika. Hii ni kwa sababu humwezesha mwanafunzi kutamka herufi kwa usahihi kwa kuziimba, na baadaye kuzisoma.

Mbinu nyingine inayotumika kujifunza kusoma na kuandika kwa sauti kama ambavyo Nadharia ya Utabia inatuelekeza ni kukariri. Mwalimu hutumia nyimbo kumkaririsha mtoto herufi mbalimbali, kutamka herufi kwa usahihi kwa kuzingatia lafudhi, matamshi ya Kiswahili sanifu, kasi stahiki katika utamkaji wa maneno, kiimbo na alama za uandishi pamoja na msamiati wa lugha husika. Kwa mfano, wimbo ufuatao humwezesha mwanafunzi kukariri herufi na kisha maneno yanayoumbwa kutokana na herufi husika:

**Iangalie Herufi**

*Iangalie kwa makini herufi,*

*sauti yake a a a na neno ni angaaa*

*Iangalie kwa makini herufi,*

*sauti yake e e e na neno ni embeee*
*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake i i i na neno ni imbaaa*
*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake o o o na neno ni ombaa*
*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake u u u na neno ni umba*

**Chanzo**: Waziri (2020)

Kupitia wimbo huu mwanafunzi anaweza kujifunza irabu **a e i o u** kwa kukariri namna zinavyotamkwa. Kwa mfano, katika sentensi isemayo "*Iangalie kwa makini herufi, sauti yake **a a a** na neno ni **a**ng**aa***" mwanafunzi hujifunza utamkaji wa irabu **a** kwa kukariri utamkaji wake kutokana na marudio ya utamkaji wa herufi hiyo kama ambavyo wanautabia wanatueleza kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha sharti ufanywe kwa kukariri na kurudiarudia matamshi ya vipande vya mazungumzo.

Pia, nyimbo humwezesha mwanafunzi kujifunza misamiati mbalimbali inayoundwa kutokana na irabu hiyo. Kwa mfano, wimbo wa **Iangalie Herufi** unaweza kumfunza mwanafunzi kusoma misamiati kama ifuatavyo:

*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake b b b na neno ni baba*

*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake c c c na neno ni chai*

*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake d d d na neno ni dada*

*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake f f f na neno ni fimbo*

*Iangalie kwa makini herufi,*
*sauti yake g g g na neno ni gari*
**Chanzo**: Waziri (2020)

Kupitia wimbo huu, mwanafunzi huzitaja herufi zote kwa kuzirudiarudia na kisha kuzikariri kwa kuzingatia utaratibu wa kialfabeti. Baadaye, uzingativu wa uundwaji wa maneno yanayotokana na alfabeti hizo hufuatia kama sehemu ya kuweka mkazo wa kuzitamka, kuzikariri na kuzitambua. Aidha, kupitia wimbo huo, wanafunzi hujifunza misamiati ya lugha husika (baba, chai, dada, fimbo na gari) kama sehemu mojawapo muhimu katika hatua za kujifunza stadi za kusoma na kuandika. Hii inatokana na kile ambacho Muaka na wenzake (2003) wanasema kuwa kabla ya mwanafunzi kujifunza kusoma na kuandika anahitaji kujifunza msamiati, sarufi na mfumo wa sauti wa lugha ya masimulizi. Wanaendelea kusema kwamba kuna muumano wa karibu sana kati ya kujifunza msamiati wa lugha fulani na uwezo wa kusoma na kuandika. Hii ina maana kuwa mwanafunzi akiwa na umilisi wa msamiati wa lugha, huwa rahisi kwake kuweza kusoma na kuandika. Kutokana na mtazamo huu, utafiti uliozalisha makala hii umebaini kuwa ili kumudu stadi za kusoma na kuandika, nyimbo ni mbinu mwafaka zaidi katika kufunza msamiati, mfumo wa lugha pamoja na sarufi kama hatua msingi za kujifunza kusoma na kuandika.

Wimbo mwingine unaofundisha utamkaji na baadaye usomaji wa maneno ni ule wa **Herufi Kuu**. Wimbo huu hutumiwa zaidi na walimu katika kiwango cha elimu cha awali ili kumfundisha mwanafunzi irabu za msingi katika suala zima la kusoma na kuandika. Msingi mkuu unaokitwa katika wimbo huu ni kwanza, kumfanya mwanafunzi apate burudani wakati anaimba na kumfanya afurahie kusoma. Pili, kumwezesha mwanafunzi kukariri irabu na kuweka kumbukumbu kama ambavyo Nadharia ya Utabia inasisitiza

kuwa kukariri na kukumbuka ni mbinu muhimu katika kujifunza kusoma na kuandika. Tatu, ni kumwezesha kutamka maneno kwa usahihi. Wimbo huo huimbwa kama ifuatavyo:

**Herufi Kuu**
*a, e, i, o, u x 2*
*Hizi ndizo herufi kuu x 2*
*Tamka kwa sauti kuu x 2*
*a, e, i, o, u x 2*
**Chanzo**: Waziri (2020)

Mwanafunzi anapoimba wimbo huu hujisikia kuburudika na wakati huohuo hujifunza kusoma kwa kuzikariri herufi, kujenga kumbukumbu na pia kutamka maneno. Skinner (1957) anabainisha wazi kuwa, licha ya ujifunzaji wa stadi mbalimbali, pia, mwigo ni uimarishaji wa tabia unaojengwa na vitia motisha. Jambo hili linasisitizwa zaidi na Jalongo (2014) anayefafanua kwamba, mchakato wa mwanafunzi kujifunza kusoma na kuandika huanzia katika burudani kuliko uelewa. Burudani huwa kama motisha kwa mwanafunzi kuangalia, kisha kusikiliza, kukumbuka, kujadili na mwisho kusoma hadithi husika. Hivyo, katika makala hii, wimbo umetazamwa kama mbinu na pia kama motisha chanya (kichocheo) inayomsukuma mwanafunzi kujifunza kusoma na kuandika.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utabia ujifunzaji wa stadi za lugha ni sawa na kujenga ujuzi wa vipashio vya lugha, kama vile fonimu, mofimu, na vifungu vya maneno ambapo kipashio kidogo hutumika kujenga kipashio kikubwa. Katika muktadha wa makala hii, kupitia nyimbo mwanafunzi huanza kujifunza kusoma na kuandika kwa huzingatia kiwango cha mwanafunzi pamoja na muktadha wa mazingira yanayomzunguka. Aidha, maneno yanayotamkwa ndani ya nyimbo lazima yazingatie vitu vinavyofahamika kwa mwanafunzi kulingana na mazingira anayoishi. Hii ina maana kuwa mwanafunzi kabla hajaanza kusoma anatarajiwa kuwa na maarifa juu ya vitu mbalimbali vinavyomzunguka katika maisha yake ya kila siku. Kinachoongezwa katika wimbo husika ni utambuzi wa irabu na konsonanti

zinazounda maneno hayo. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa uundaji wa maneno haufanani kati ya eneo moja na lingine. Aidha, ujifunzaji wa irabu na konsonanti pamoja na uundaji wa maneno huzingatia mazingira husika ili kumsaidia mwanafunzi kupata urahisi wa kusoma na kuandika kwa kuhusianisha anachojifunza kupitia wimbo na mazingira yake. Mfano mwingine wa wimbo unaotumika kufundishia stadi za kusoma ni huu ufuatao:

**Ndege Mtini**

*Ndege mtini porini wamelala,*

*Wa kwanza akaruka akasema* ***a***

*Wa pili akaruka akasema* ***e***

*Wa tatu akaruka akasema* ***i***

*Wa nne akaruka akasema* ***o***

*Wa tano akaruka akasema* ***u***

*Wa sita akaruka akasema* ***a e i o u***

*Wote wakaruka juu, juu, juu zaidi*

**Chanzo**: Waziri (2020)

Wakati wa uimbaji wa wimbo huu wanafunzi huruka kwa kupokezana huku kila mmoja akitamka herufi mojamoja. Uimbaji huo hufanywa kwa kurudiwarudiwa na kukaririwa mpaka pale mwanafunzi anapoweza kutamka irabu zote kwa usahihi. Pia, uimbaji wa pamoja huwashirikisha wanafunzi wote kuzitamka kwa pamoja irabu hizo. Utamkaji wa namna hii huwaunganisha hata wale ambao uwezo wao wa kujifunza ni mdogo. Hivyo, huwasaidia kukaririsha irabu na konsonanti za Kiswahili na hatimaye kuweza kusoma neno, sentensi na hata tungo.

Kwa kawaida, maneno ya Kiswahili huundwa na konsonanti na irabu, ingawa yapo machache ambayo yanaweza kuundwa na irabu pekee. Hivyo, mwanafunzi anapojifunza irabu hizi na kuzielewa ni hatua muhimu sana katika kumwezesha kusoma na kuandika silabi na hatimaye kuunda neno zima. Utafiti umebaini kwamba upo urahisi wa kusoma endapo wimbo utatumika kukaririsha wanafunzi irabu ama konsonanti fulani. Hii inatokana na ukweli kwamba wimbo humsaidia mwanafunzi kuwa na kumbukumbu ya kudumu juu ya irabu na konsonanti zinazounda neno au sentensi kwa ujumla.

### 4.2.2 Nyimbo Zitumikazo Kufundishia Kuandika

Kuandika ni stadi ya kuweka mawazo katika maandishi kwa ajili ya kusomwa (TET, 2016). Kama ilivyo katika stadi za kusoma, kuandika pia huhitaji mafunzo maalumu kwa mwanafunzi anayeanza kujifunza ili aweze kuandika kwa kiwango cha kuridhisha. Stadi za kuandika hujengwa na umahiri mahususi unaojumuisha: uumbaji wa herufi, ushikamani na kuandika kwa ufasaha sentensi sahili.

Ili mwanafunzi aweze kujifunza umahiri mahususi kama ilivyobainishwa hapo awali ni lazima ajue sifa na maumbo mahususi ya kila irabu na konsonanti. Zipo nyimbo mbalimbali ambazo hutumiwa kufundishia stadi za kuandika. Nazo ni zile zinazotumika kuwaelekeza wanafunzi namna ya kuumba herufi kwa kuanza na hatua ya mwanzo hadi ya mwisho. Hatua za uumbaji wa herufi zinaweza kufanywa kwa wimbo unaobainisha sifa ya herufi hiyo kwa kuifananisha na umbo la kitu.

Kama ambavyo Nadharia ya Utabia inatueleza kuwa kujifunza lugha ni sawa na kujenga ujuzi wa vipashio vya lugha kama vile fonimu, mofimu, na hatimaye vifungu vya maneno. Mbinu ya nyimbo hutumika kufunza sifa na maumbo ya irabu na konsonanti mbalimbali kama vipashio vya kisarufi ambavyo huunda silabi, neno, sentensi hadi tungo. Miongoni mwa nyimbo zinazotumiwa zaidi na walimu kufundishia herufi mbalimbali na hatimaye kumwezesha mwanafunzi kujua kuandika ni pamoja na huu ufuatao:

**Hii Ndiyo A**

*Hii ndiyo a,*
*aaa inamkia mrefu aaa*

*Hii ndiyo e,*

*eee iko kama kata eee*

*Hii ndiyo i,*
*iii ina kofia Kichwani iii*

*Hii ndiyo o,*
*ooo iko kama yai ooo*

*Hii ndiyo u,*
*uuu imekaa kama kikombe uuu*

**Chanzo**: Waziri (2020)

Wimbo huu humsadia mwanafunzi kujua kuandika kwa namna kuu tatu. Kwanza ni motisha ambayo humpa burudani na kumfanya asichoke wala kukata tamaa pale anapojifunza. Pili, humwezesha kukariri maumbo ya herufi anazojifunza kwa urahisi kwa kuzihusianisha na maumbo halisi ya vitu vinavyopatikana katika mazingira yake. Kwa mfano, anapoimba kwa kutamka herufi *u* na kuihusianisha na kikombe ni rahisi kwa mwanafunzi kuiandika herufi hiyo kwa kuvuta taswira ya kikombe na hivyo kuiweka katika maandishi. Tatu, wimbo humwezesha mwanafunzi kujenga kumbukumbu ya kudumu na hivyo kusoma kwa urahisi. Stadi ya kuandika huhitaji pia mwanafunzi kuwa na kumbukumbu nzuri ili kupata muunganiko wa kile anachojifunza. Anapohusisha umbo la herufi *e* na kata, hataweza kusahau kwa urahisi kwani kila atakapotaka kuandika herufi hiyo dhana ya umbo la kata itamjia kichwani. Kinachosisitizwa katika zoezi zima la kujifunza kusoma na kuandika kupitia nyimbo za namna hii ni mwalimu kutumia sifa ya vitu vinavyopatikana katika mazingira ya wanafunzi kama ambavyo imesisitizwa katika Nadharia ya Utabia. Hii inatokana na ukweli kuwa, sifa za kila irabu hubadilika kulingana na mazingira ya ujifunzaji. Kwa mfano, irabu *e* baadhi ya walimu huifananisha na nyoka na wengine huifananisha na kata. Pia, irabu *i* wengine husema imekaa kama fimbo na wengine husema ina kofia kichwani. Kutofautiana huko kunatokana na

namna mwalimu alivyoamua atumie sifa ipi itakayomsaidia mwanafunzi wake kuelewa kwa urahisi. Hivyo, mwalimu anapaswa kubuni sifa ya maumbo mbalimbali yanayofahamika vyema kwa mwanafunzi ili kurahisiha ufundishaji na ujifunzaji. Pia, kumwezesha mwanafunzi kuelewa kila anachojifunza kwa urahisi.

Kwa kutumia wimbo kama kichocheo kinachomtia mtoto ari ya kupenda kuandika, kumwondolea uchovu na pia kumjengea kumbukumbu akilini, mwanafunzi huweza kuandika maumbo mbalimbali ya herufi kwa kukariri hatua mbalimbali anazopaswa kufuata wakati wa uandikaji wa herufi hiyo. Mfano mzuri wa wimbo unaofunza hatua za uandikaji wa herufi ni wimbo wa **Maumbo ya Sauti**. Huu humwezesha mwanafunzi kujifunza stadi ya kuandika kwa kumfanya atambue hatua mbalimbali anazopaswa kufuata wakati anaandika herufi husika. Nao huimbwa kama ifuatavyo:

**Maumbo ya Sauti**

*Kuandika napenda maumbo ya sauti, mwalimu niwezesheee*

*Kwa kuliumba umbo la sauti ya a,*
*hatua nne fuataaa*
*Moja…, mbili…, tatu..., nne…,*

*Kwa kuliumba umbo la sauti ya e,*
*hatua mbili fuataaa*
*Moja…, mbili…,*

*Kwa kuliumba umbo la sauti ya i,*
*hatua tatu fuataaa*
*Moja…, mbili…, tatu…*

*Kwa kuliumba umbo la sauti ya o,*
*hatua mbili fuataaa*
*Moja…, mbili…*

*Kwa kuliumba umbo la sauti ya u, hatua nne fuataaa*
*Moja…, mbili…, tatu…, nne….*
**Chanzo**: Waziri (2020)

Mwanafunzi anapoimba wimbo huu, huongozwa kufanya hatua mbalimbali za uandishi wa herufi hewani, mchangani au daftarini. Hatua hizo huzingatia namna anavyopaswa kuanza kuandika herufi, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano, anapoimba, "Kwa kuliumba umbo la sauti ya *a*, hatua nne fuataaa" na kisha kuanza kutaja namba "Moja…, mbili…, tatu..., nne…". Hutaja namba hizo huku akionesha kwa vitendo hatua mbalimbali za uandishi wa herufi tajwa mpaka itakapokamilika. Kwa kufanya hivyo, kwanza mwanafunzi hukariri umbo la herufi husika na kuwa rahisi kwake kuiandika. Pili, humrahisishia ujifunzaji wa uandishi wa herufi husika kwa kuziandika huku akifuata hatua za uandishi wa herufi hiyo. Hapa wimbo huchukua nafasi ya burudani ambapo mwanafunzi hujifunza na wakati huohuo akiburudika. Huchukua nafasi ya motisha na kumfanya apende kujifunza kuandika kwa kurudiarudia na hivyo kurahisisha tendo la kuandika. Pia, huvuta umakini wa mwanafunzi katika kujifunza.

## 5.0 Hitimisho

Kupitia makala hii imebainika kuwa nyimbo kama kipengele kimojawapo cha fasihi ya watoto ya Kiswahili ni mbinu mwafaka katika kufundishia stadi za kusoma na kuandika. Hii inatokana na namna inavyojihusisha na suala zima la ufundishaji na ujifunzaji kama sehemu kuu ya motisha kwa mwanafunzi. Pia, imebainika kuwa, nyimbo hutumiwa kama mbinu ya kumkaririsha mwanafunzi maumbo na sauti za herufi mbalimbali. Vilevile, ni mbinu muafaka katika kujenga kumbukumbu kwa watoto; lakini pia, hutumika kama burudani inayomfanya mwanafunzi ajifunze pasipo kuchoka, na hivyo, kuweza kumudu stadi za kusoma na kuandika kwa urahisi. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa fasihi ya watoto ya Kiswahili katika kujifunza, kuimarisha na kukuza stadi za kusoma na kuandika, mpaka sasa hakuna mwongozo rasmi uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na

Teknolojia ukielekeza namna ya kuitumia fasihi ya watoto ya Kiswahili kama mbinu ya kufundishia kusoma na kuandika.

Kutokana na umuhimu wa fasihi ya watoto katika kukuza stadi za kusoma na kuandika, kama ilivyobainishwa na makala hii, kwanza, inapendekezwa kuwa watunga sera watazame upya mbinu zenye ufanisi zinazoweza kutumika kufundishia stadi za kusoma na kuandika na kuziingiza katika mitaala ya elimu. Miongoni mwake ni mbinu ya nyimbo ambayo kupitia makala hii imeonekana kuwa na ufanisi mkubwa. Ikumbukwe kuwa utoaji wa elimu bora ni pamoja na kuhakikisha kuwa watu wanaoisoma elimu hiyo wanakuwa na ujuzi wa kusoma na kuandika. Kwa hiyo, ni wajibu wa serikali na wizara husika kuhakikisha kuwa kunakuwapo na nyimbo maalumu ambazo zitatumika katika kukuza stadi hizo. Miongozo iliyopitiwa na watafiti inadokeza tu kuwa nyimbo zitumike kufundishia madarasa ya awali, lakini haibainisha ni nyimbo zipi zinazoweza kutumika kufundishia kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Pili, watunzi wa vitabu vya watoto wanapaswa kulitazama suala la fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa jicho la kipekee. Mapendekezo haya yanatokana na ukweli kuwa vitabu vya nyimbo za watoto za Kiswahili havijapewa umuhimu kwa shule za msingi. Hata hivyo, walimu hutumia uzoefu na ubunifu wao kuzitumia kufundishia kusoma na kuandika. Hali hii ikiachwa iendelee, kuna hatari kubwa ya kuibuka kwa tofauti ya uelewa wa wanafunzi wa sehemu moja na wale wa sehemu nyingine.

## Marejeleo

Abdallah, S. (2018). *Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano Kutoka katika Vibonzo Jongevu*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapwa), Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Bakize, L. H., Lyimo E. B., na Ngugi, P. M. (2017). Maendeleo ya Fasihi ya Watoto ya Kiswahili Nchini Tanzania na Kenya: Mkabala Linganishi. *Kiswahili*, 80, 115 – 136.

Chacha, S. R. (2016). *Uhusiano wa Mikakati ya Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Umilisi wa Kusoma katika Shule za Msingi Kasarani Kaunti ya Nairobi Kenya*, Tasinifu Uzamili (Haijachapwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.

Darton, F. J. (1982). *Children's Books in England: Five Centuries of Social Life*. Cambridge: Cambridge University Press.

Jolongo, M. (2014). *Young Children and Picture Books.* U.S.A: National Association for the Education of Young Children.

Khakasa, L. S. (2018). *Mikakati ya Kufundisha Stadi za Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi*. Kakamega. The African Premier Research Publishing Hub.

Muaka, A., Pang, E. S, na Kamili, E. (2003). *Kufundisha Kusoma: Mfululizo wa Mazoea ya Kielimu 12.* Brussels: Ufaransa na SADAG Bellegrade.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Ngugi, P. (2010). *Language and Literacy Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Kenya.* Berlin: Lambert Academic Publishing.

__________ (2009). The Children's Literature Research in Kenyan Universities: Where are We Now? *International Journal of Arts and Commerce*, 1 (2), 101-110.

Omari, S. (2009). Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania, *Kiswahili*, 71, 101-110.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu.* Dodoma: Central Tanganyika Press.

Sanders, J. (1967). *Psychological Significance of Children's Literature: The Library Quartely.* USA: The University of Chicago Press.

Shima, G. (2012). Nafasi ya Vielelezo katika Fasihi ya Watoto. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapwa), Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.

Skinner, B. F. (1957). *Verbal Behaviour*. New York: Appleton.

TET. (2016). *Mwongozo wa Mwalimu Kufundisha Elimu Awali*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

TET. (2018). *Mwongozo wa Mwalimu Kufundisha Elimu Awali*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Watson, S. M., Gable, R. A., Gear, S. B., & Hughes, K. C. (2012). Evidence- based Strategies for Improving the Reading Comprehension of Secondary Students: Implications for Students with Learning Disabilities. *Learning Disabilities Research & Practice*, *27*(2), 79.

Waziri, S. (2020). Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kiswahili katika kukuza Stadi za Kusoma na Kuandika: Uchunguzi wa Nyimbo za Watoto (haijachapwa), Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.